FUNZO LA 1

-Kwa nini nilikuja hapa?
-Je, nilikuja hapa kukuumiza?
-La.
-Je, nilikuja hapa kuiumiza familia yako au marafiki wako?
-La.
-Je, nilikuja hapa kuiba mashamba au ng'ombe wenu?
-La.
-Kwa nini nilikuja hapa?
-Nimekuja hapa kwa jambo moja pekee.

-Nimekuja hapa kukueleza ujumbe muhimu zaidi ulimwenguni.
-Nimekuja hapa kukueleza ujumbe wa Mungu.

-Sikuja kukueleza ujumbe wa mzungu.
-Sikuja hapa kukueleza ujumbe wa mtu mweusi.

-Nimekuja hapa kukueleza tu ujumbe wa Mungu.

-Kama chifu wenu angewaita nyote pamoja kwa ujumbe muhimu, je, mngekuja?
-Ndiyo, mngekuja.

-Kwa nini mngekuja?
-Kwa sababu chifu angekuwa na ujumbe muhimu wa kuwaeleza.

-Ujumbe wa chifu ni muhimu, lakini kuna ujumbe ulio muhimu zaidi.



-Ni ujumbe wa nani ulio muhimu zaidi ya ujumbe wa chifu?
-Ujumbe wa Mungu.

-Ni ujumbe wa nani ulio muhimu zaidi ulimwenguni?
-Ujumbe wa Mungu.

-Kwa nini ujumbe wa Mungu ndiyo ujumbe muhimu zaidi ulimwenguni?

-Kwa sababu ni Mungu pekee ambaye hajawahi kudanganya.
-Kwa sababu ni Mungu pekee ambaye amekuwa akisema ukweli wakati wote.

-Ni nani kati ya watu ambaye hajawai kudanganganya?
-Watu wote wamedanganganya.

-Ni nani kati yenu ambaye hajawai danganya?
-Nyote mshawahi kudanganya.

-Pia mimi nimewahi kudanganya hapo awali.

-Wazungu wote wamedanganya.
-Watu weusi wote wamedanganya.
-Watu wote wamedanganya.

-Nani peke yake hajawahi kudanganya?
-Mungu.
-Kwa sababu Mungu hajawahi kudanganya, Mungu pekee ndiye anayeweza kutuambia ukweli.

-Kwa sababu Mungu hajawahi kudanganya, Mungu pekee ndiye anayeweza kutuambia ukweli kumhusu Mungu.

-Kwa sababu Mungu hajawahi kudanganya, ujumbe wake ndiyo ujumbe muhimu zaidi ulimwenguni kote.

-Kwa wanaume, ujumbe wa Mungu ni muhimu zaidi ya kufanaya kazi shambani.
-Kwa nini?
-Kwa sababu ni ujumbe wa Mungu peke yake ndiyo unaoweza kuokoa wanaume wote kutokana na kifo.

-Kwa wanawake, ujumbe wa Mungu ni muhimu zaidi ya kupika chakula.
-Kwa nini?
-Kwa sababu ni ujumbe wa Mungu pekee ndiyo unaoweza kuokoa wanawake kutokana na kifo.

-Kwa watoto, ujumbe wa Mungu ni Muhimu zaidi ya kucheza.
-Kwa nini?
-Kwa sababu ni ujumbe wa Mungu pekee ndiyo unaoweza kuokoa watoto kutokana na kifo.

-Ujumbe wa Mungu uko wapi?
-Ujumbe wa Mungu umo katika kitabu cha Mungu.

-Jina la kitabu cha Mungu ni lipi?
-Jina la kitabu cha Mungu ni Biblia.

-Ujumbe wa Mungu uliingia aje katika kitabu cha Mungu?



-Mungu alikuwa na uwezo wa kuandika kitabu chake yeye mwenyewe, lakini Mungu hakufanya hivyo.

-Hapo zamani, Mungu aliwachagua baadhi ya watu, kisha akatia maneno yake katika mawazo ya hao watu.

-Kisha hao watu wakayaandika maneno ya Mungu ndani ya kitabu cha Mungu.

-Je, hao watu waliandika maneno yao ndani ya kitabu cha Mungu?
-La.
-Hao watu ambao Mungu aliwachagua, hawakuandika maneno yao.

-Hao watu ambao Mungu aliwachagua, waliandika tu maneno ya Mungu.

-Hao watu, ambao Mungu aliwachagua, waliyaandika maneno ya Mungu hakika kama vile walivyoambiwa na Mungu.

-Mungu aliwachagua watu arubaini ili waandike maneno yake ndani ya kitabu chake.

-Je, hao watu ambao waliandika maneno ya Mungu, wote waliishi katika wakati mmoja?
-La.

-Hao watu ambao waliandika maneno ya Mungu, hawakuishi wote katika wakati mmoja.

-Je, ilichukuwa miaka mingangapi kuandika maneno yote ya Mungu?

-Iliwachukuwa muda wa miaka 1,600 watu ambao Mungu aliwachagua kuandika maneno yake.

-Hao watu ambao Mungu aliwachagua kuandika maneno yake ni nani?

-Watu ambao Mungu aliwachagua kuandika maneno yake walikuwa Wayahudi na Myunani.

-Je, hawa watu waliandika maneno ya Mungu kwa lugha gani?
-Kwa lugha ya Kiyahudi na ya Kiyunani.

-Je, hao watu waliandika maneno ya Mungu kwa lugha ya Kiingereza?
-La.
-Je, watu hao waliandika maneno ya Mungu kwa lugha ya Kiarabu?
-La.
-Je, watu hao waliandika maneno ya Mungu kwa lugha ya Kifaransa?
-La.

-Hao watu waliandika maneno ya Mungu kwa lugha zao.

-Kwa sababu watu hao waliochaguliwa na Mungu kuandika maneno yake walikuwa Wayahudi na Myunani mmoja.



-Hao watu walindika maneno ya Mungu kwa lugha ya Kiyahudi na Kiyunani.

-Baadaye, watu wengine walienda katika nchi ya Wayahudi, wakasoma maneno ya Mungu, kasha wakaandika katika lugha zao.

-Maneno ya Mungu yametafsiriwa kwa lugha nyingi za ulimwnguni.

-Maneno ya Mungu hivi sasa yanatafsiriwa kwa lugha yako.

-Ni maneno ya Mungu mangapi katika kitabu cha Mungu ambayo ni ya kweli?
-Yote.

-Mbona maneno yote ya Mungu katika kitabu cha Mungu ni ya kweli?

-Kwa sababu Mungu kamwe hadanganyi.
-Kwa sababu Mungu husema ukweli pekee.

-Mbona twaweza kuwamini maneno yote ya Mungu katika kitabu chake?

-Kwa sababu Mungu kamwe hadanganyi.
-Kwa sababu Mungu hunena ukweli pekee.

-Ni nani ambaye wakati wote husema ukweli?
-Mungu.

-Nimeyasoma maneno ya Mungu katika kitabu cha Mungu na najua kuwa maneno yote ya Mungu ni kweli.

-Ukiyasikiliza maneno ya Mungu, utajua kuwa maneno yote ya Mungu ni kweli.

-Hii ni kwa sababu kamwe Mungu hadanganyi.
-Hii ni kwa sababu Mungu hunena ukweli pekee.

-Mungu ana mengi ya kutuambia.
-Kwa hivyo, itachukua siku nyingi kukufundisha maneno ya Mungu.

-Ufuatao ni mfano:
-Inachukua siku ngapi kujifundisha ukulima?
-Siku nyingi.
-Mbona inachukua siku nyingi kujifundisha ukulima?

-Kwa sababu kuna kweli nyingi za kujifundisha kuhusu ukulima.
-Lazima ujue jinsi ya kuandaa shamba.
-Lazima ujue jinsi ya kupanda mbengu.
-Lazima ujue jinsi ya kupalilia kwekwe.
-Lazima ujue jinsi ya kuvuna mazao.

-Kama vile inavyochukua siku nyingi kujua ukulima, ndivyo inavyochukuwa pia siku nyingi kujua maneno ya Mungu.

-Hii ni kwa sababu kuna kweli nyingi katika maneno ya Mungu.



-Ukiyasikiliza maneno ya Mungu siku nyingi, utajua kweli nyingi kumhusu Mungu.

-Ufuatao ni mfano mwingine:
-Je, wewe hula chakula kila siku?
-Ndiyo.
-Mbona wewe hula chakula kila siku?
-Kwa sababu mwili wako unahitaji chakula kila siku.

-Kama vile mwili wako unahitaji chakula kila siku, ndivyo pia wewe unavyohitaji kuyasikiliza maneno ya Mungu kila siku.

-Kama huli chakula kila siku, nini kitakachofanyika?
-Utakufa.
-Kama huyasikilizi maneno ya Mungu kila siku, pia utakufa.

-Mbona baadhi ya watu hawajui ujumbe wa Mungu?

-Kwa sababu watu hawa wanakataa kuusikiliza ujumbe wa Mungu.
-Kwa sababu watu hawa wanakataa kuamini ujumbe wa Mungu.

-Kama utayasikiliza maneno ya Mungu kila siku, utakuwa na furaha.
-Kama hautayasikiliza maneno ya Mungu kila siku, utakuwa na huzuni.

-Natumai kwamba utakuja kusikiliza maneno ya Mungu kila siku.